



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

MAMILAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA

**TAARIFA YA UKAGUZI WA DAWA, VIFAA TIBA NA VITENDANISHI KATIKA
VITUO VYA FORODHA
2021- 2022**

KANDA YA MASHARIKI

Dfco

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba, TMDA Kanda ya Mashariki
P. O. Box 31356, Jengo la Victoria, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, Dar es Salaam
Tel: +255-737-226328/788470301, Fax: +255-22-2450793
Website: www.tmda.go.tz, Email: info.eastzone@tfda.go.tz

1.0 UTANGULIZI

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ina jukumu la kulinda afya ya jamii kwa kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa bidhaa za dawa (binadamu na mifugo), vifaa tiba na vitendanishi.

Taarifa hii inaonesha utekelezaji wa kazi ya ukaguzi wa bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika kipindi cha mwaka 2021/22 uliofanywa na Ofisi ya Kanda ya Mashariki katika vituo vya forodha vilivyopo Bandari ya Dar es Salaam, Bandari Kavu za Dar es Salaam (ICDs), Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, mpaka wa Horohoro na Bandari ya Tanga

2.0 LENGO LA UKAGUZI

Ukaguzi ulilenga kubaini ubora na usalama wa bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi kabla ya kuruhusiwa kuingizwa, kusambazwa, kuuzwa au kutumika nchini hususani;

- 2.1 Kubaini endapo bidhaa zinakidhi vigezo vya ubora na usalama vinavyotakiwa.
- 2.2 Kubaini na kujiridhisha kuwa bidhaa sio bandia.
- 2.3 Kubaini uwepo wa bidhaa zilizokwisha muda wake wa matumizi au zisizofaa kwa matumizi.
- 2.4 Kubaini iwapo muda wa kuisha matumizi uliobaki kwenye bidhaa husika unakubalika kwa mujibu wa Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba Sura 219.
- 2.5 Kuhakikisha kuwa bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi zinazoingizwa nchini zina vibali vya TMDA.
- 2.6 Kujiridhisha iwapo bidhaa zinakidhi matakwa ya Kanuni za Uwekaji lebo ambapo pamoja na lugha zingine bidhaa inatakiwa kuwa na lugha za kingereza au kiswahili au zote kwa pamoja.

3.0 HATUA YA UTEKELEZAJI

Katika kipindi hiki, Kanda ya Mashariki ilifanya kaguzi za dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya forodha kwa mikoa ya Dar es Salaam na Tanga. Jumla ya shehena **9,030** zenye thamani ya **USD 1,131,898,523.69** zilikaguliwa katika Bandari ya Dar es Salaam, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) na mpaka wa Horohoro, Bandari ya Tanga kwa mchanganuo ufuataao;

Na.	Aina ya bidhaa	Shehena zilizokaguliwa	Thamani (USD)
1.	Dawa	5,502	748,047,544
2.	Vifaa tiba na vitendanishi	3,488	376,992,014
3.	Malighafi za dawa	39	6,601,565.69
4.	Malighafi za Tumbaku	1	257,400
Jumla		9,030	1,131,898,523.69

Kaguzi za bidhaa katika vituo vya forodha na mipaka zilibaini baadhi ya mapungufu ikiwa ni pamoja na baadhi ya bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi kutokukidhi matakwa ya lebo, uwepo wa bidhaa za dawa na vifaa tiba ambazo hazijasajiliwa, baadhi ya bidhaa za dawa na vifaa tiba kukaribia kuisha muda wake wa matumizi au kukutwa umeisha na baadhi ya waingizaji kuletaa bidhaa za dawa na vifaa tiba nchini bila ya kuwa na vibali vya TMDA. Pia mizigo inayoingizwa nchini kwa masharti ya kuteketezwa kushindwa kuteketezwa kwa wakati.

Hata hivyo Kanda ya Mashariki inaendelea kutoa elimu kwa waingizaji wa bidhaa nchini juu ya matakwa ya Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura 219.

4.0 MAFANIKIO

Mafanikio mbalimbali ya udhibiti yamepatikana ambayo ni pamoja na:

- 4.1 TMDA Kanda ya Mashariki, imefanikiwa kuwa na wakaguzi katika vituo vyote vya forodha waliopata mafunzo ili kudhibiti ubora na usalama wa bidhaa za dawa na vifaa tiba zinazoingizwa nchini na kuweza kutoa huduma kwa wateja wake kwa wakati.
- 4.2 Matumizi ya mfumo wa kielektroniki unaowasadida wateja kuomba vibali na kuvipakua wenye kutoka kwenye mfumo bila ya kufika kwenye Ofisi za TMDA hivyo kupunguza muda na gharama kwa wateja tunaowahudumia.
- 4.3 Kufanya kazi kwa kushirikiana na wadau wengine kama Mamlaka ya Mapato (TRA), Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) hivyo kuweza kutatua changamoto mbalimbali tunazokutana nazo katika kaguzi na hatimaye kuhakikisha kuwa huduma kwa wateja zinatolewa kwa wakati.

5.0 HITIMISHO

TMDA Kanda ya Mashariki inaendelea kufanya kaguzi za bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi vinavyoingia nchini ili kuhakikisha kuwa zinakidhi matakwa ya Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba Sura 219. Aidha inatoa rai kwa wananchi pale ambapo watawabaini wanaofanya biashara ya bidhaa za dawa, vifaa tiba na vitendanishi kinyume na sheria wasisite kutoa taarifa TMDA kwa ajili ya ufuatiliaji.

IMEANDALIWA NA TMDA KANDA YA MASHARIKI


A. A. BITEGEKO
MENEJA WA KANDA